JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA YA WILAYA YA SIMANJIRO KWA MH.KASSIM MAJALIWA (MB) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA ZIARA YAKE TAREHE 16 FEBRUARI 2017

IMEANDALIWA NA OFISI YA MKUU WA WILAYA
S.L.P 9503
ORKESUMET
SIMANJIRO
Email: das.simanjiro@manyara.go.tz

1.0 UTANGULIZI

1.1 SURA YA WILAYA

Wilaya ya Simanjiro ni kati ya Wilaya tano (5) zinazounda Mkoa wa Manyara. Wilaya ilianzishwa mwaka 1993 ikimegwa kutoka wilaya ya Kiteto. Wilaya inapakana na wilaya ya Monduli upande wa Kaskazini Magharibi, wilaya za Arumeru, Hai na Moshi upande wa kaskazini, Kiteto upande wa kusini, Kondoa na Babati upande wa Magharibi na Mwanga, Same, Kilindi na Korogwe upande wa Mashariki. Wilaya ina eneo lenye jumla ya kilometa za mraba **20,591**.

1.2 JIOGRAFIA NA HALI YA HEWA YA WILAYA

Wilaya iko katika eneo la nyanda kame na mbuga, hivyo hupata mvua za wastani wa kati ya milimita **400** na **500** kwa mwaka. Wilaya ina vipindi viwili vya mvua ambavyo ni vuli na masika. Mvua za vuli hunyesha kuanzia mwezi Novemba hadi Desemba na masika hunyesha kuanzia mwezi Machi hadi Mei**.**

1.3 UTAWALA, IDADI YA WATU NA PATO LA MWANANCHI

Wilaya ya Simanjiro ina Tarafa sita **(6),** Kata kumi na nane **(18),** Vijiji hamsini na saba (**57)** na Vitongoji mia mbili themanini na moja (**281).** Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ilikuwa na jumla ya wakazi **178,693**, kati yao Wanawake ni **89,718** na Wanaume **88,975**.Kwa mwaka 2017 Wilaya inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi **211,746,** kati yao wanawake **106,313** na wanaume **105,433** sawa na ongezeko la asilimia **3.2** kwa mwaka**.**

Hali ya uchumi katika Wilaya ya Simanjiro inaendelea kukua kwa wastani. Pato la Mkazi (D-GDP) kwa mwaka 2010 lilikuwa shilingi **268,000** na mwaka 2015 lilikadiriwa kufikia Shilingi **455,000**. Shughuli kuu zinazowapatia kipato wakazi wa Simanjiro ni pamoja na Ufugaji, Kilimo, Uchimbaji wa Madini, Uvuvi, Utalii na Viwanda vidogo vidogo. Mwelekeo wa wilaya ni kuhimiza na kuhamasisha maendeleo kwa wananchi kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuinua pato la mwananchi wa wilaya kufikia wastani wa kitaifa wa pato la Mtanzania.

1.4 HALI YA ULINZI NA USALAMA WILAYANI

Hali ya ulinzi na usalama katika Wilaya ya Simanjiro ni ya kuridhisha kwani hakuna matukio makubwa ya kutisha isipokuwa uhalifu mdogo mdogo unaodhibitiwa na vyombo vya ulinzi na usalama. Mahusiano ya vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama kama Polisi, Mahakama, mabaraza ya kata pamoja na vyombo vya utawala na uwakilishi wa wananchi ni ya kuridhisha kutokana na mamlaka za Vijiji, Kata na Tarafa kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. Kunapokuwepo na viashiria vya migogoro hushughulikiwa mapema na mamlaka ya Wilaya na kupatiwa ufumbuzi stahiki. Wilaya haina migogoro ya kidini, kisiasa wala ukabila.

1.5 HALI YA OFISI YA MKUU WA WILAYA

Hali Ya Watumishi

Ofisi ina watumishi **12** kati ya **44** wanaohitajika sawa na **asilimia 27** ya mahitaji, watumishi waliopungua ni Maafisa Tarafa wawili (**02**), mhasibu mmoja (**01**) Wasaidizi wa Kumbukumbu saba (**07**), wasaidizi wa ofisi saba **(07)** walinzi **(10)** Makatibu Muhtasi saba **(07**).

Aidha, pamoja na upungufu huo wa kiikama uliopo hitaji kubwa la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa sasa ni watumishi wa Kada za Maafisa Tarafa **(02),** Makatibu Muhtasi **(02),** Dereva (**01**) na Msaidizi wa Kumbukumbu (**01),** hii ikiwa sawa na asilimia **19** ya upungufu uliopo.

1.6 MALI NA MAJENGO OFISI YA MKUU WA WILAYA

Ofisi ina magari mawili moja kwa matumizi ya Mkuu wa Wilaya **STL 2430** na jingine kwa matumizi ya utawala **STK 3773** magari yote ni mazima na yanatembea. Aidha kuna pikipiki mbili za Maafisa tarafa wa tarafa za Moipo na Naberera ambazo zinatembea lakini chakavu. Ofisi ya mkuu wa wilaya inamiliki majengo 3 ambayo ni Rest house ilipo nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya, nyumba ya makazi ya Katibu Tawala na nyumba ya makazi ya watumishi. Wilaya haina jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

1.7. HALI YA WATUMISHI KATIKA HALMASHAURI

Halmashauri ina jumla ya watumishi **1,441** katika Idara **13** na vitengo **6.** Aidha, Halmashauri inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi wapatao **579** kutoka katika idara na vitengo mbalimbali ambao wameombewa kibali cha ajira katika bajeti ya 2016/17. Kipaumbele cha wilaya ni kupata watumishi wa idara za elimu na afya ambao wanahitajika kwa kiasi kikubwa kutokana na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na la kwanza pamoja na mahitaji ya kupeleka huduma za afya kwa kila kijiji.

Kutokana na kuchelewa kutolewa kwa kibali cha ajira, halmashauri imeendelea kutumia gharama kubwa kwa kuajiri watumishi wa mkataba wa muda mfupi hasa Maafisa watendaji wa vijiji na wahudumu. Hadi kufikia **31 Januari, 2017** Halmashauri ina jumla ya watendaji wa vijiji **14** walioajiriwa kwa mkataba wa muda mfupi wa hadi miaka mitatu na wahudumu **6,** watumishi hawa wanaigharimu halmashauri kwa kiasi kisichopungua **Tshs 4,200,000** kila mwezi.

2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATIKA WILAYA

Wilaya ya Simanjiro inaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kuzingatia sera na miongozo mbalimbali ya kitaifa kama vile Mpango wa matokeo makubwa sasa (BRN), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano, hotuba ya Rais wakati wa ufunguzi wa Bunge la 11 na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/17. Utekelezaji huu unafanywa kupitia sekta

mbalimbali za vipaumbele kama ifuatavyo;

2.1. SEKTA YA BARABARA

Wilaya ya Simanjiro ina Mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa **1,388.67**. Kati ya hizo kilometa **580** ni barabara za Mkoa na Kilometa **808.67** ni barabara za Wilaya. Mtandao wa barabara za Wilaya unajumuisha kilometa **294.6** za Wilaya, kilometa **430.5** barabara za vijijini, kilometa **83.57** barabara za Mji na Vivuko ni **293** kwa mchanganuo wa Kalvati **240** na Drift **53**. Aidha Halmashauri haina hata kilometa moja ya barabara ya lami. Barabara za changarawe ni kilometa **145.85** na barabara za udongo ni kilometa **667.67** Katika utekelezaji wa mpango na bajeti wa **2016/2017** na **2017/2018**, Wilaya itaweza kuboresha miundombinu ya barabara kwa kilometa **612**,zitakazogharimu kiasi cha Tsh **2,179,935,502.01**. Hii itawezesha Wilaya kuongeza wastani wa barabara zinazopitika muda wote kutoka ya sasa asilimia **40.2** hadi kufikia asilimia 45, iwapo fedha zote zitatolewa na kwa wakati tofauti na kipindi cha 2015/16 ambapo mfuko wa Barabara haukuleta bajeti hivyo kukwamisha mpango wa uboreshaji miundombinu ya barabara

2.2 SEKTA YA ELIMU

Wilaya ya Simanjiro ina jumla ya shule **87** za Msingi, kati ya hizo **79** ni za Serikali na **8** za watu binafsi. Jumla ya Shule za Msingi **65** zinatoa elimu ya awali. Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha shule zote za Msingi zinakuwa na madarasa ya elimu ya awali. Pia Wilaya ina Shule za Msingi **3** za bweni ambazo ni Naberera, Simanjiro na Ruvu Remiti.

2.2.1 Uandikishaji wa wanafunzi

(i) Elimu ya awali

Katika mwaka **2016/2017**, Wilaya ililenga kuandikisha wanafunzi **3,920** katika madarasa ya elimu ya awali, Wasichana **1,845** na Wavulana **2,035**. Hadi tarehe 31, 2017 Wilaya ilikuwa imeandikisha jumla ya wanafunzi **2,708** kati yao wasichana **1,263** na wavulana **1,445**, sawa na asilimia **69** ya watoto waliotarajiwa kuandikishwa kwa mwaka. Uhamasishaji na uandikishaji wa wanafunzi bado unaendelea.

(ii) Darasa la kwanza

Katika mwaka **2016/2017**, Wilaya ililenga kuandikisha wanafunzi **6,225** wa darasa la kwanza, ikiwa wasichana **2,969** na wavulana **3,256**. Hadi tarehe 31, Januari 2017, Wilaya iliweza kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza **5,781**, Wasichana **2,730** na Wavulana **3,051,** sawa na asilimia **92.8** ya watoto waliotarajiwa kuandikishwa kwa mwaka. Kumekuwa na hamasa na mwitikio mkubwa wa uandikishaji kutokana na sera ya serikali ya elimu bure. Hadi kufikia Desemba 2016 wanafunzi **6,938** wa darasa la kwanza walikuwa wameandikishwa sawa na ongezeko la wanafunzi **1,429** katika kipindi kama hicho mwaka 2015 ambapo wanafunzi **5,509** walikuwa wameandikishwa. Hili ni sawa na ongezeko la **asilimia 26**.

2.2.2 Matokeo ya mtihani wa darasa la vii kwa mwaka 2016

Katika mtihani wa darasa la saba **2016**, wanafunzi **3,069** walisajiliwa kufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi, wasichana ni **1,555** na Wavulana **1,514**. Wanafunzi **3,034** ikiwa wasichana **1,538** na Wavulana **1,496** walifanya mtihani wa kuhitimu darasa la Saba sawa na asilimia **99** ya wanafunzi waliosajiliwa. Wanafunzi **1,507** kati ya hao Wasichana **730** na Wavulana **777** walifaulu Mtihani wa Taifa sawa na asilimia **49.7**. Wilaya imesikitishwa na ufaulu duni na tayari imeweka mikakati mbalimbali ili kuboresha ufaulu kufikia asilimia **80** kwa mwaka **2017**. Wanafunzi **9** walichaguliwa kujiunga na shule za sekondari za bweni za kitaifa na **1,498** walichaguliwa kujiunga na shule za Sekondari za Kutwa.

Ufaulu huu ulizingatia wastani wa alama kuanzia **100-250**. Hata hivyo, wanafunzi **35** kati yao wasichana **18** na wavulana **17** hawakufanya mtihani kwa sababu mbalimbali ikiwemo utoro, Ugonjwa na vifo.

2.2.3 Hali ya miundombinu ya shule za msingi

Hali ya miundombinu katika shule nyingi za msingi si ya kuridhisha kutokana na upungufu wa madarasa **305**, vyoo **755** na nyumba za walimu **515**. Wilaya imejipanga kukabiliana na upungufu wa miundombinu hiyo kwa mwaka **2016/17** kwa kukamilisha ujenzi wa madarasa **47,** nyumba za walimu **10** na vyoo **100** kwa kutumia fedha za mapato ya ndani, ruzuku ya maendeleo na wadau wa maendeleo wilayani. Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Wilaya imetenga jumla ya **Tsh.461,113,460** ili kuboresha miundombinu ya Elimu msingi kwa kujenga madarasa **14**, nyumba za walimu **11** na vyoo **100.** Hivyo ifikapo Juni **2018**, Wilaya itakuwa imekabiliana na upungufu wa madarasa kwa zaidi ya asilimia **20**, nyumba za walimu asilimia **5** na Vyoo asilimia **26**.

2.3 ELIMU SEKONDARI

Wilaya ina jumla ya shule za sekondari **16** kati ya hizo shule **15** ni za serikali na moja ni ya binafsi. Shule hizo zina jumla ya Wanafunzi **4,353** kati yao wavulana **2,218** na wasichana **2,135.**

2.3.1 Upokeaji wanafunzi kidato cha kwanza mwaka 2017

Wilaya ina uwezo wa kupokea wanafunzi **1,920.** Wanafunzi **1,507**, kati yao wavulana **777** na wasichana **730** walichaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza. Wanafunzi **9** kati yao Wavulana **7** na Wasichana **2** walichaguliwa kujiunga na shule za bweni nje ya Wilaya. Hadi tarehe 31 Januari **2017**, Wanafunzi **1106** kati yao wasichana **526** na Wavulana **580** wameripoti katika shule walizopangiwa sawa na asilimia **74** ya waliochaguliwa. Ufuatiliaji unaendelea ili kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaripoti.

2.3.2. Matokeo ya Mtihani wa Taifa kidato cha nne 2016

Watahiniwa **868** kati yao wavulana **445** na wasichana **423** walifanya mtihani wa CSEE **2016,** sawa na asilimia **99** ya Wanafunzi waliosajiliwa. Ufaulu wao ni kama unavyoonekana katika jedwali namba 1 linalofuata hapa chini.

Jedwali namba 1. Takwimu za waliofanya mtihani na madaraja ya ufaulu mwaka 2016.

MWAKA	WALIOFANYA	MADARAJA					% UFAULU
		DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	DIV. 0	
2016	868	6	43	135	443	241	72%

Kiwango cha ufaulu Kiwilaya kimeendelea kupanda kutoka asilimia **47** (**2014**), asilimia **61 (2015)** hadi kufikia asilimia **72.24** (**2016**). Sawa na ongezeko la asilimia **25** katika kipindi cha miaka miwili. Wilaya inatarajia kuwa kiwango cha ufaulu kitapanda zaidi watahiniwa wa mwaka **2017** watakapofanya mitihani yao.

2.3.3. Matokeo ya Mtihani wa Taifa kidato cha pili 2016

Halmashauri ya Wilaya ilikuwa na jumla ya Shule **16** zilizofanya mtihani wa kidato cha pili Novemba, **2016.** Shule **15** ni za serikali na moja ni shule binafsi (Mgutwa Sekondari). Jumla ya Watahiniwa **1,124** walifanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha pili. Matokeo yao ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali namba 2 hapa chini.

Jedwali namba 2. Matokeo ya Mtihani wa Taifa kidato cha ii mwaka 2016

WALIOFANYA MTIHANI			MADARAJA YA UFAULU (VISION)					% Ufaulu	% Kufeli
WAV	WAS	JUMLA	Distinction	Merit	Credit	Pass	Fail		
562	**562**	**1124**	**109**	**174**	**273**	**514**	**54**	**95**	**5**

Kiwango cha ufaulu kwa mtihani wa kidato cha pili kwa miaka miwili mfululizo (**2015** na **2016**) kimekuwa kile kile yaani **asilimia 95**. Hata hivyo jitihada zaidi katika ufundishaji na kuwapa muda wa kutosha wanafunzi kujisomea na kazi kwa vitendo utatolewa ili kuinua kiwango cha ufaulu katika matokeo ya Mwaka **2017** Wilaya ifikie **asilimia 100.**

2.3.4. Hali ya miundombinu katika shule za sekondari

Katika kuhakikisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia yameboreshwa, Wilaya katika mwaka **2016/17** imepanga kutumia shilingi **187,727,000** kuwezesha ujenzi wa mabweni **3,** Nyumba za Walimu **2,** maabara **1** na choo cha matundu **8.** Pia jitihada zinafanyika kuhimiza wananchi kuchangia nguvukazi ili kuwezesha miradi hii kukamilika kwa wakati.

Aidha, katika mwaka wa fedha **2017/2018**, Wilaya imetenga bajeti ya **Tsh.258,000,000** ili kuboresha miundombinu ya Elimu ya Sekondari, hii ikiwa ni kamilisha ujenzi wa Madarasa **2** mabweni **2** maabara **1** vyoo **4** vya matundu **8** na nyumba za walimu **1.** Kwa kuwa Wilaya haina shule ya kidato cha tano na sita, ukamilishaji wa mabweni **2** na Madarasa **2** katika shule za Emboreet na Orkesumet kutaifanya wilaya kuwa na shule mbili za kidato cha kidato cha tano na sita.

2.4. SEKTA YA AFYA

Wilaya ya Simanjiro hadi sasa haina hospitali ya wilaya. Kuna hospitali moja inayomilikiwa na Kanisa la KKKT ambayo iko katika hatua za mwisho za kuingia Mkataba na Halmashauri ya Wilaya ili kuwezesha Wilaya kuwa na hospitali ya Wilaya itakayojulikana kama hospitali teule ya Wilaya. Kutokana na hali hiyo, huduma za Afya Wilayani bado zinatolewa kwa kutumia Zahanati na Vituo vya Afya. Hadi sasa Wilaya ina jumla ya Vituo vya Afya Vinne **(4),** Kati ya hivyo vituo vitatu **(3)** vya serikali na kimoja **(1)** cha taasisi ya dini, zahanati **35** kati ya hizo **29** za serikali, **2** za binafsi na **4** za taasisi za dini. Wilaya ina mpango wa kupandisha hadhi kituo cha afya Urban Orkesumet kuwa Hospitali ya Wilaya. Ili kuhakikisha hilo, kiasi cha **Tsh 620,000,000/=** kimetengwa katika bajeti ya 2017/18 kwa ajili ya kuanzisha na kukamilisha ujenzi wa wadi sita (wanawake 2,wanaume **1**,watoto **2,** Jengo **1** la utawala na chumba cha kuhifadhi maiti). Ujenzi huu ukikamilika kituo hicho kitaanza kutoa huduma za Hospitali ya Wilaya.

(i) Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba

Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutoa huduma za afya ni ya kuridhisha hasa kutokana na serikali kuendelea kutoa fedha kupitia mfuko wa pamoja wa afya (health sector basket fund). Kuanzia Julai 2016 hadi Januari 2017, wilaya imeshapokea awamu tatu ya fedha za mfuko wa afya kiasi cha **Tshs. 483,890,250** ambapo asilimia **33** ilielekezwa kwenye ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Licha ya kupata fedha hizo, kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa dawa zote zinazohitajika kutoka bohari kuu ya madawa (**MSD**) kutokana na kutakiwa kuwasilisha maombi kwa muda maalumu ili kuwezesha bohari kufanya manunuzi kulingana na mahitaji. Bohari ya madawa imekuwa ikitoa barua pale inapokosa dawa na vitendanishi husika ili wilaya iweze kununua kwenye maduka ya dawa. Hivyo, kutokana na manunuzi ya dawa yaliyoyofanyika kwa fedha za awamu hizo tatu, wilaya imepunguza kwa kiasi kikubwa kero ya upungufu wa dawa.

(ii) Hali ya maambukizi ya VVU

Kwa upande wa maambukizi ya VVU Wilaya inaendelea na zoezi la kuhamasisha jamii kujitokeza na kupima maambukizi ya Virusi vya Ukimwi. Hadi kufikia **Januari 31, 2017,** Jumla ya Wananchi **6,323** wakiwemo wanawake **4,224** na wanaume **2,099** wamejitokeza kupima afya zao. Hata hivyo Watu **225** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **3.5** ya wananchi waliojitokeza kupima afya zao. Aidha kwa wale waliogundulika kuwa na maambukizi ya VVU wamepewa ushauri nasaha ili kuanza kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU. Kwa upande wa maeneo hatarishi, wilaya imeweka uzito wa kipekee katika mikakati yake ya kupambana na maambukizi ya VVU kwenye Mji Mdogo wa Mirerani ambako kiasi cha maambukizi kilikuwa **asilimia 16** mwaka **2015** lakini hadi kufikia **31, Januari, 2017** jumla ya wananchi **773** wakiwemo wanawake **563** na wanaume **180** walijitokeza kupima afya zao.Hata hivyo watu **85** waligundulika wakiwa na maambukizi ya VVU kati yao wanawake **60** na wanaume **25** sawa na **asilimia 11.** Mikakati inayotumika katika eneo

hili ni pamoja na kuendelea na uhamasishaji wa jamii kwa kutumia washauri rika na wataalamu wa idara ya afya, kugawa mipira ya kiume ya kujikinga pamoja na upimaji na utoaji wa dawa za kufubaza VVU.

(iii) Huduma ya mama na mtoto

Wilaya imeendelea kutoa huduma za mama na mtoto katika vituo vyote **39** vya kutolea huduma kwa lengo la kupunguza vifo vya kina mama wajawazito na watoto ili kufikia lengo la kitaifa. Hata hivyo, changamoto kubwa ni elimu duni kwa kina mama wa jamii za kifugaji ambao hujifungulia majumbani na wakati mwingine kufikishwa kituoni wakiwa na hali mbaya kiasi cha kuhatarisha uhai wao na watoto wao.

Huduma kwa wazee imeendelea kutolewa katika vituo vyote vya kutolea huduma kwa kuwapa kipaumbele wazee wenye umri wa kuanzia miaka **60** kwa kuwa na dirisha lao maalum la kupatia tiba, hadi sasa jumla ya Wazee **909** ikiwa wanawake **507** na wanaume **402** wamepokelewa na kupewa huduma mbalimbali za matibabu hapa Wilayani.

(iv) Hali ya upatikanaji wa damu salama

Wilaya inaendesha zoezi la uchangiaji na ukusanyaji wa damu salama ambalo husimamiwa na timu ya damu salama ya wilaya inayoongozwa na mtaalamu wa maabara wa wilaya. Zoezi hili limeanza rasmi mwezi **Oktoba 2016** na hadi kufikia **31, Januari 2017**, kiasi cha unit **81** zilikuwa zimekusanywa. Damu hii inasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto hasa wakati wa kujifungua. Kampeni ya ukusanyaji damu inaendelea kwa mpango unaoratibiwa na idara ya afya ya Halmashauri.

2.4.1 Mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa (iCHF)

Wilaya ya Simanjiro inaendelea na uhamasishaji wa jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF). Wananchi wamekuwa na mwitikio mzuri kwa kujitokeza kujiunga na mfuko huo. Hadi **31 Januari**, **2017** jumla ya wananchi **546** sawa na kaya **91** wameshajiandikisha kujiunga na mfuko, ikiwa sawa na asilimia **3.6** ya Malengo. Kwa kuzingatia kuwa zoezi limeanza tarehe **31 Disemba 2016**, mwitikio huu ni mzuri kwani matarajio ni kupata kaya **15,000** ifikapo mwezi **Desemba 2017**.

2.5 MAPATO YA HALMASHAURI

(i) Ruzuku na miradi ya maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilikasmia kukusanya jumla ya **Tshs**. **21,775,006,000** kutokana na vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo;

CHANZO	MAKISIO	UTEKELEZAJI JULAI–JANUARI 2017	ASILIMIA
Mapato ya ndani	2,330,427,000.00	930,502,478.35	40
Fidia ya kodi	161,094,330.88	36,555,000.00	23

Ruzuku za kawaida(OC)	1,506,797,669.12	172,503,199.00	11
Ruzuku ya mishahara (PE)	12,970,230,000.00	7,931,969,500.00	61
Miradi ya maendeleo	5,003,923,010.00	2,702,639,511.76	54
JUMLA	**21,972,472,010.00**	**11,774,169,689.11**	**54**

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Januari 2017, serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo elimu, afya na miundombinu ya barabara. Jumla ya shilingi **224,000,000** zimepokelewa na kuelekezwa kwenye uboreshaji wa miundombinu ya elimu na afya hasa ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, ujenzi wa wadi ya wazazi kituo cha afya Orkesumet na ukarabati wa jengo la kituo cha afya Mirerani. Shilingi **483,890,250** zimepokelewa kupitia mfuko wa pamoja wa afya na kutumika kulingana na mwongozo wake na kiasi cha shilingi **700,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya. Eneo la ujenzi lipo tayari na hatua inayoendelea ni usanifu wa michoro na maandalizi ya mchanganuo wa gharama unaofanywa na wakala wa Majengo (TBA) Mkoa wa Manyara.

(ii) Uboreshaji wa mapato ya ndani ya halmashauri

Kwa upande wa mapato ya ndani Wilaya ilikuwa imekadiria kukusanya shilingi **2,330,427,000** ambapo hadi kufikia 31,Januari,2017 jumla ya **Tshs 930,502,478.35** zilikusanywa sawa na asilimia **40.** Halmashauri imeendelea kubainisha vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo lililokusudiwa. Baadhi ya mikakati ni pamoja na kutumia mawakala kukusanya kodi ya huduma kwa makampuni ya madini ambayo yamekuwa na mwitikio hafifu wa kulipa pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa makusanyo katika vyanzo vya mapato vilivyopo ili kuziba mianya ya upotevu. Aidha, halmashauri inakusanya na kusimamia mapato kutoka vyanzo vyote badala ya vijiji ambavyo vilikuwa vikikusanya kwa utaratibu wa kurejesha asilimia 20 ya makusanyo hayo kwenye vijiji husika.

2.6 SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

Wilaya inatambua na imejipanga kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa taifa kupitia sekta ya viwanda ambayo imeainishwa katika ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ibara 32 (g) uk.27, kwa kubainisha fursa za uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Kwa upande wa viwanda vidogo, kila kijiji kimeelekezwa kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda na biashara ndogondogo. Wilaya imebainisha vijiji vyenye fursa za uanzishaji viwanda na kuanza kuvijengea hamasa ya wenyeji kuanzisha viwanda hasa vya mazao ya mifugo kama vile viwanda vya maziwa, ngozi, viatu na nyama. Vijiji hivyo ni Naberera, Terat, Endiamtu, Shambarai, Lorimorjio, Kityangare na Sukuro. Wananchi

katika vijiji hivi wataandaliwa mafunzo maalumu kwa uratibu wa idara za kilimo, mifugo na biashara.

2.6.1 Utengaji wa maeneo ya uwekezaji

Wilaya imekwishapima eneo la EPZ, Eneo hili liko ndani ya Kata za Shambarai na Endiamtu, lina jumla ya Ekari **1,311**. Michoro na ramani ya eneo hilo imekwisha idhinishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Wilaya imeanza kulitangaza eneo hilo katika makongamano na warsha mbalimbali zilizofanyika nje na ndani ya Mkoa wa Manyara. Hata hivyo jukumu la kutafuta wawekezaji ni la mamlaka ya EPZ na wilaya iko tayari kutoa ushirikiano kadri itakavyohitajika. Uwepo wa eneo hili, utachochea shughuli za kiuchumi wilayani na kufungua fursa za ajira kwa wananchi pamoja na kukuza vipato vyao.

2.6.2 Viwanda na biashara

Wlaya inatekeleza sera ya ukuzaji wa uchumi kuelelekea uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda na biashara kama zilivyoainishwa katika sura ya 2 sehemu ya 32 (uk. 25) ya ilani ya Chama cha Mapinduzi **(CCM)** ya mwaka 2015. Kwa upande wa fursa za kibiashara, wilaya imeshaainisha mashamba makubwa yanayozidi **ekari 50** ambayo yako **88**. Mashamba haya yanaweza kutumika kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo na biashara na kuongeza malighafi katika viwanda vya kusindika mazao ya nafaka. Kwa kutumia mazao ya mifugo kama vile ngozi, nyama, maziwa na pembe/kwato, wilaya ina fursa za kualika wadau kuwekeza katika viwanda vya usindikaji wa nyama, utengenezaji wa bidhaa za ngozi na viwanda vya maziwa. Wilaya imetenga maeneo ya viwanda katika mji mdogo wa Mirerani na Orkesumet kwa ajili ya vikundi vya wajasiriamali vijana yenye ukubwa wa **meta za mraba 7,639** katika mji mdogo wa Orkesumet na **ekari 10** kwa Mirerani.

Wilaya ilikuwa na **viwanda 3** vya maziwa katika maeneo ya Naberera, Terrat na Orkesumet na machinjio ya kisasa ambavyo hata hivyo vilisimama uzalishaji wake kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu wa masoko na gharama za uendeshaji kuwa kubwa. Wilaya imepanga kujadiliana na waliokuwa wamiliki na waendeshaji wa viwanda hivyo kuvifufua kwani mazungumzo ya awali na baadhi yao hasa shirika la IYOPA yameonyesha kuwa bado wana nia hiyo.Wilaya ina malengo ya kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo **18** kwa uwiano wa kiwanda kimoja kwa kila kata hasa vinavyotumia malighafi zinazotokana na mazao ya mifugo.

2.7 SEKTA YA MAJI

2.7.1 Aina na idadi ya vyanzo vya maji.

Wilaya ya Simanjiro inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kuhakikisha jamii inapata maji safi na salama si zaidi ya **mita 400**. Hadi tarehe **31, Januari 2016**, Wilaya ilikuwa na aina sita (6) ya vyanzo vya maji vyenye uwezo wa kuhudumia asilimia **52** ya wakazi wote Wilayani.

Wilaya katika kuhakikisha kwamba asilimia ya wananchi wanaopata maji safi na salama inaongezeka kutoka **asilimia 52** ya mwaka **2014** hadi **54** ifikapo mwaka **2018,** Wilaya inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kuchimba, kujenga na kusambaza maji katika **Vijiji 7**. Kazi ya ukamilishaji na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji imekamilika katika Vijiji **4** ambapo wananchi **11,917** wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji. Miradi iliyobaki ya Vijiji **3** itaendelea mara baada ya Wilaya kupokea fedha kutoka Serikali kuu. Hata hivyo hati zenye thamani ya **Tsh 488,487,503.01** za madai ya Wakandarasi hao imewasilishwa wizarani kwa ajili ya kukamilisha taratibu, kwa ajili ya malipo.

2.7.2 Mradi wa maji kutoka Mto Ruvu hadi Mji wa Orkesumet

Zaidi ya **asilimia 90** ya wakazi wa Mji wa Orkesumet wanatumia maji yenye Chumvi/Magadi. Hata hivyo jitihada mbalimbali zimefanyika ili kuhakikisha jamii inapatiwa maji baridi. Moja ya jitihadi hizo ni kuibuliwa kwa Mradi wa Maji kutoka mto Ruvu hadi Mji wa Orkesumet. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya maendeleo ya watu wa Uarabuni kwa gharama ya **dola million 16** na serikali inachangia **dola milioni 2** na hivyo kufanya jumla ya **dola milioni 18** hadi utakapokamilika. Mradi unatekelezwa kwa awamu mbili kwa muda wa miezi kumi na nane kuanzia mwezi Januari 2017. Wizara ya maji na umwagiliaji ndiye msimamizi mkuu wa mradi huu kwa ushauri wa pamoja wa kampuni ya kigeni ya SHOURA CONSULT LTD ya Sudan na Interconsult ya Dar es Salaam.

Kampuni ya JANDU PLUMBERS ndiyo iliyoshinda zabuni ya awamu ya pili ya ujenzi wa mradi huu inayohusisha utandazaji wa mabomba kutoka kwenye chanzo hadi mji wa Orkesumet na ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji huku zabuni ya awamu ya kwanza ikiwa katika hatua za mwisho. Mradi huu ukikamilika utakuwa na uwezo wa kutoa maji lita **1,500,000** kwa siku na kuweza kuhudumia jumla ya Wakazi wapatao **27,762** wa mji wa Orkesumet na Vijiji vya Jirani na hivyo kuondoa kwa kiasi kikubwa kero ya muda mrefu ya wananchi wa Orkesumet na vijiji vya jirani.

2.8. SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

2.8.1 Aina na idadi ya mifugo

Zaidi ya asilimia **80** ya wakazi wa wilaya ya Simanjiro ni wa jamii ya kifugaji. Hadi kufikia tarehe **31 Januari, 2017** Wilaya ilikadiriwa kuwa na mifugo **1,102,899** inayojumuisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, mbwa na nguruwe, ngamia na kuku. Hata hivyo idadi hii imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuzaliana kwa mifugo na kuhamia kutoka wilaya nyingine. Taarifa hizi hupatikana kwa kutumia zoezi la chanjo mbalimbali zilizofanyika pamoja na takwimu zinazotolewa na serikali za Vijiji husika mwaka hadi mwaka. Hivyo, hadi kufikia tarehe **31 Januari, 2017** idadi ya mifugo iliyopo Wilayani inaoneshwa katika jedwali **Na. 3** lifuatalo hapo chini.

Jedwali namba 3. Idadi ya Mifugo

KOSAAFU/MIFUGO	AINA NA IDADI YA MIFUGO							
	NG'OMBE	MBUZI	KONDOO	NGURUWE	PUNDA	KUKU	MBWA	NGAMIA
ASILI	437,925	396,452	225,003	895	21,867	94,428	7,240	59
ILIYOBORESHWA	15,487	29,455	32,946	-	-	6,603	-	-
JUMLA	453,412	425,907	257,949	895	21,867	101,031	7,240	59

2.8.3 Miundombinu ya mifugo

Miundombinu ya mifugo iliyopo wilayani ni michache na mingine inahitaji ukarabati ili kuboresha afya ya mifugo katika Wilaya. Baadhi ya miundombinu iliyopo ni kama ifuatavyo:-

(i) Majosho

Katika wilaya ya Simanjiro kuna jumla ya Majosho **25** kati ya hayo, majosho mazima ni **24** na josho moja ni bovu linahitaji ukarabati mkubwa. Josho hili liko katika eneo lililokuwa ranchi ya zamani eneo la Olmot kata ya Terrat na Komolo, hivyo halifikiki kwa urahisi. Majosho haya yamekuwa hayafanyi kazi vizuri mwaka mzima kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na:-kuhitaji ukarabati mkubwa, kukosekana kwa maji/Ukame katika maeneo mengi na wafugaji kushindwa kuchangia fedha za uogeshaji ili josho liweze kujiendesha.

Kutokana na umbali kati ya kijiji hadi kijiji kunatakiwa baadhi ya vijiji vyenye mifugo mingi kujengewa majosho ili kusogeza huduma hiyo. Hivyo Wilaya ina upungufu wa majosho **8** ambayo yangejengwa katika vijiji vya Loibosoit A, Losinyai, Kitwai A/Loonderkes, Olerumo, Kilombero, Laangai, Oiborkishu/Lorokare na Endiamtu. Majosho hayo yangepunguza msongamano wa mifugo katika maeneo mengine.

(ii) Malalambo na mabwawa

Wilaya ina jumla ya malambo/mabwawa **51** yakijumuisha malambo ya asili na yale ya kuchimbwa. Mabwawa mengi yamekuwa hayawezi kuhifadhi maji kwa muda mrefu kutokana na kutokuwa makubwa, wingi wa mifugo na wakati mwingine mvua kunyesha kwa kiwango cha chini. Hali hii imekuwa ikisababisha adha kubwa kwa wafugaji na mifugo yao hususani kipindi cha kiangazi. Kutokana na idadi ndogo ya mabwawa na mengi kutokuwa na ukubwa wa kuhifadhi maji kwa muda mrefu wilaya ina upungufu wa mabwawa makubwa takribani **20** katika maeneo mbalimbali ya wafugaji. Katika mwaka wa fedha **2016/17** wilaya ina mpango wa kukarabati bwawa **moja** la Langai na kuomba ushirikiano wa wadau wa sekta ya mifugo kuchimba mabwawa **3** ili kukabiliana na changamoto hii.

(iii) Vibanio

Wilaya ina jumla ya vibanio vya kudumu **9**, majosho yaliyokarabatiwa na yanatumika kama vibanio **6** na vibanio vya muda ambavyo hutengenezwa wakati wa chanjo **58** kati ya vibanio **114** vinavyohitajika. Vibanio hivi ni vya muda na vinakabiliwa na changamoto ya kutokidhi vigezo na mahitaji. Hivyo kuna haja kutokana na mazingira ya wilaya kuwa na vibanio viwili vya kudumu katika kila kijiji. Wilaya inaendelea na uhamasishaji wa wananchi katika vijiji husika kushiriki katika ujenzi na ukarabati wa vibanio ili kukabiliana na upungufu huo.

(iv) Machinjio

Wilaya ina machinjio mawili (**2)** yaliyoko katika miji midogo ya kata za Orkesumet na Mererani. Huduma ya uchinjaji inahitaji kuwa na makaro ya kuchinjia katika maeneo rasmi ya vijiji. wilaya inaendelea kuhamasisha na kusimamia ujenzi na ukarabati wa vichinjio **16** kwa kata zilizobaki na **makaro 57** kwa uwiano wa karo 1 kila kijiji.

(v) Vituo vya Afya ya Mifugo

Wilaya ina kituo kimoja cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kilichopo makao makuu ya wilaya. Katika kuboresha huduma ya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo, vituo viwili vimeanzishwa katika kata za Emboreet na Naisinyai, ambavyo vitaanza kufanya kazi hivi karibuni baada ya kuwekewa umeme. Kuna maduka ya pembejeo za mifugo **36** ya watu binafsi wilayani ambayo yamekuwa yakitegemewa na wafugaji kwa kupata madawa na pembejeo nyingine za mifugo.

2.8.4 Huduma za mifugo.

(i) Uboreshaji wa mifugo

Katika jitihada za uboreshaji wa mifugo ili kumletea mfugaji tija jitihada mbalimbali zinafanyika. Moja ya jitihada hizo ni uanzishwaji wa vituo vya uhamilishaji na ununuzi wa madume bora ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na majogoo ili kuboresha koostafu zetu za asili na kuongeza uzalishaji na ubora. Mwitikio umekuwa ni mkubwa katika suala hili baada ya wafugaji wenyewe kuona tofauti ya ndama/mfugo ulioboreshwa na ndama/ mifugo ya asili. Kupitia miradi ya DADPs, TASAF, wahisani (VECO, Wold Vission, Heifer International) na wafugaji wenyewe. Jumla ya mifugo ifuatayo ilinunuliwa na ndama kuzaliwa.

Jedwali namba 4. Mifugo iliyonunuliwa

Ng'ombe (Sahwal, Boran,)			**Mbuzi (Isiolo, Togenberg, Saanan)**			**Kondoo (BHP)**		
Madume	Majike	Ndama	Madume	Majike	Ndama	Madume	Majike	Ndama
1,006	**5,011**	**7,476**	**3,862**	**10,808**	**10,943**	**3,080**	**15,793**	**9,776**

Hadi kufkia Desemba 2016, vituo **3** vya **uhamilishaji** vilianzishwa vikiwa na jumla ya wataalamu **5.** Wahudumu wa Mifugo ngazi ya Jamii **(WAMIJA)** 18 walipatiwa mafunzo ya uhamilishaji kupitia DADPs na shirika lisilo la kiserikali la WORLD VISSION. Zoezi la Uhamilishaji limekuwa likisuasua kutokana na mwitikio mdogo wa wafugaji, wengi kushindwa kuchangia gharama na pia ng'ombe wengi kutokana na lishe na mazingira hawaonyeshi dalili za joto kiurahisi.

(ii) Udhibiti , chanjo na matibabu ya magonjwa ya mifugo

Magonjwa mengi ambayo yamekuwa yakisumbua wafugaji ni magonjwa yaenezwayo na kupe na mbung'o (kama vile Ndigana kali, Ndigana baridi, Maji moyo, Mkojo damu, Ormillo, Nagana) vilevile CBPP, CCPP, FMD, BQ, Anthrax, LSD, PPR, Minyoo, Ukurutu, TB, Orf, NCD, Fowl Pox na Nairobi Sheep disease. Baadhi ya magonjwa haya kuna yanayodhibitiwa kwa chanjo, mengine kwa kuogesha mifugo na mengine hayana kinga na inabidi kufanya matibabu pindi yanapotokea. Upatikanaji wa chanjo za kutosha na kwa wakati kwa chanjo zinazotolewa na Serikali, gharama za chanjo na uchanjaji imekuwa changamoto kubwa katika kudhibiti magonjwa.

2.8.5 Uvuvi

Wilaya ya Simanjiro ina mabwawa 2 ambayo shughuli za uvuvi zinafanyika. Mabwawa hayo ni Nyumba ya Mungu na Kidapash. Uvuvi katika mabwawa haya umekuwa ukifanyika katika kipindi chote cha mwaka. Changamoto kubwa katika mabwawa haya ni matumizi ya zana haramu za uvuvi (Vikirerwe, makokoro, migono, vyandarua/mitengo) ambazo zimepelekea kuvuliwa kwa samaki wadogo chini ya nyanda tatu. Kutokana na kukithiri kwa uvuvi haramu kiasi cha kusababisha samaki kupungua sana Serikali za mikoa ya Manyara na Kilimanjaro zilikubaliana kufunga bwawa la Nyumba ya Mungu kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2017 ili kuruhusu samaki kuzaliana.

Tangu wakati huo hadi sasa Halmashauri imeendelea kufanya doria na kukamata wavuvi wanaoendelea kuvua samaki kwa wizi na kuwachukulia hatua mbalimbali zikiwemo kuchoma zana zao, kushikilia nyenzo za usafirishaji kama magari na pikipiki na kuwafungulia mashtaka katika mahakama ya wilaya. Hadi kufikia Desemba 2016, jumla ya makokoro **44** na nyavu za kutega **12** zilikamatwa na kuteketezwa, pikipiki **21** zilikamatwa kati yake 10 zilitozwa faini ya shilingi 500,000 kila moja **2** hazijalipiwa na **9** bado zinashikiliwa kutokana na mashauri yaliyoko mahakamani. Aidha magari 8 yalikamatwa na kati yake magari **3** yalitozwa faini ya shilingi **3,500,000** kila moja na 1 shilingi **1,000,000** na yaliyobaki yameshikiliwa kutokana na kuwa na kesi mahakamani au wamiliki wake kukimbia na kutojitokeza hadi sasa. Aidha jumla ya mitumbwi **10** na vyandarua **4** vilikamatwa na kuteketezwa. Kwa upande wa samaki, jumla ya ndoo **358** zilikamatwa kati yake ndoo **300** ziligawanywa katika taasisi mbalimbali kama vile shule za sekondari Nyumba ya Mungu na Msitu wa Tembo pamoja na gereza la Karanga

lililoko Moshi. Kutokana na faini na tozo mbalimbali, halmashauri ilipata jumla ya shilingi **16,500,000** kati ya Julai hadi Desemba 2016.

2.9. SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

Wilaya inakadiriwa kuwa na ekari **346,000** zinazofaa kwa kilimo cha mazao ya biashara na chakula. Kati ya hizo, takribani ekari **144,000** hutumika kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara sawa na asilimia **41.**

2.9.1 Hali ya mvua

Katika kipindi hiki cha vuli wilaya imepata mvua kiasi cha milimita za ujazo **28.7** zilizonyesha mwishoni mwa mwezi Novemba na mwanzoni mwa Desemba, 2016. Hii ni chini ya wastani wa mvua za vuli kwa mwaka ambazo huwa kati ya milimita 150 hadi 200

2.9.2 Hali ya kilimo

- Kiasi cha ekari **115,000** (hekta **46,000)** hutumika kwa kilimo cha nyanda kame. Mazao ambayo hulimwa katika eneo hili ni pamoja na mahindi, maharage na ngwara katika eneo kubwa na alizeti, mtama na ufuta katika maeneo madogo.

- Kilimo cha umwagiliaji kinahusisha maeneo yaliyopo katika bonde la Mto Pangani ikiwa ni pamoja na maeneo ya Lemkuna, Msitu wa Tembo, Ngage, Kiruani, Loiborsoit B, Ruvu Remiti na Gunge. Maeneo mengine ni pamoja Shambarai, Kambi ya Chokaa, Kilombero na Zaire.

- Katika kuboresha matumizi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, elimu ya matumizi sahihi imeendelea kutolewa kwa wakulima kupitia jumuia za watumia maji. Vijiji **12** vina eneo la ekari **29**,**000** (hekta **11,600)** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo ni ekari **7,725** (hekta **3,090)** tu ndizo zinatumika

- Katika mwaka **2016/2017** Wilaya inatekeleza Miradi ya umwagiliaji yenye thamani ya **Tsh.bil. 1.8**.Ni matumaini yetu kuwa miradi hii katika vijiji vya Ngage,Lemkuna na Kambi ya chokaa ikikamilika itaongeza eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta **3,090** za sasa hadi **5,275** hivyo kuongeza eneo la umwagiliaji kwa **asilimia 58.6**.

2.9.5 Tathmini ya hali ya usalama wa chakula

Hali ya usalama wa chakula katika kipindi hiki si ya kuridhisha. Hali hii inadhihirishwa na upungufu wa mzunguko wa nafaka mahindi sokoni na kwenye baadhi ya vijiji. Aidha, bei ya mazao sokoni hususani zao la mahindi imepanda na kufikia wastani wa **Tshs 95,000/=** kwa gunia la kilo mia moja. Zao la maharage kwa gunia la kilo mia moja limefika wastani wa **Tshs 145,000** hadi **180,000/=.** Kupanda kwa bei ya mazao hasa zao la mahindi haikuwahi kutokea kwa miaka mingi sasa. Hali hii

inaonyesha dalili kuwa baadhi ya maeneo katika wilaya na hasa yale ambayo hayakupata mvua za kutosha katika msimu huu yatakumbwa na upungufu wa chakula. Maeneo hayo ni pamoja na kata za Ngorika, Msitu wa Tembo, Oljoro Namba 5 na Komolo. Jumla ya kaya **5,441** zenye watu **15,709** wa maeneo hayo zinahitaji chakula kinachokadiriwa kufikia **tani 1,226** kuanzia mwezi Februari hadi Mei **2017**.

2.9.7 Pembejeo msimu wa 2016/17

Katika msimu wa 2016/2017 wilaya imepatiwa pembejeo za kilimo zenye ruzuku ya serikali kiasi cha tani **10** za mbegu za mahindi aina ya chotara na tani **40** za mbolea ya kukuzia. Pembejeo hizi kupitia kikao cha Kamati ya Pembejeo ya wilaya zimeelekezwa katika maeneo ya kilimo cha umwagiliaji. Tayari makampuni yameainishwa na serikali na mawakala wamekwishateuliwa kwa ajili ya kusambaza pembejeo.

2.10 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

2.10.1Mikopo ya Wanawake na Vijana.

Wilaya imeendelea kutekeleza mpango wa kuwakopesha wanawake na vijana kulingana na miongozo ya kitaifa. Katika mwaka wa fedha **2015/16** jumla ya vikundi vine **(4)** vya wanawake viliweza kukopeshwa kiasi cha Tsh. **26,400,000** katika kata za Endonyongijape, Shambarai na Orkesumet ikiwa ni mkopo pamoja na riba ya asilimia **10.** Urejeshwaji wa fedha hizo bado haujanza kwani muda wao wa kuerejesha bado haujakamilika kwavile marejesho yataanza Machi **2017**.

Kwa upande wa vijana, jumla ya vikundi sita (6) katika kata za Loiborsoit, Orkesumet na Endonyongijape vilikopeshwa kiasi cha Tsh. **26,400,000** ikiwa ni mkopo pamoja na riba ya asilimia kumi **(10%).** Hali kadhalika, vikundi vya vijana havijanza kurejesha kwani muda wa kufanya urejeshaji haujafika, wataanza kurejesha kuanzia mwezi Machi **2017**. Kwa mwaka **2016/17** wilaya imepokea maombi ya vikundi vya vijana na wanawake **24** vinavyohitaji mikopo yenye thamani ya shilingi **milioni 320** na tayari jumla ya shilingi **milioni 21** zimeshatolewa kwa vikundi **4** vya wanawake na vijana kati ya shilingi **208,862,940** zilizotengwa.

Vikundi vya vijana vilivyopata mkopo ni Manyara Environmental Group cha Mirerani kwa shilingi **4,000,000** na Juhudi Group cha Orkesumet kwa shilingi **8,000,000**. Kwa upande wa wanawake vikundi vilivyopata ni KIWASU cha Gunge kilichopata shilingi **3,000,000** na Namnyaki cha Terrat kilichopata shilingi **6,000,000.**

Hata hivyo Wilaya bado inaendelea na uchambuzi wa vikundi vingine vya wanawake na vijana kulingana na mwongozo wa kitaifa wa mfuko wa maendeleo ya wanawake kwa lengo la kuvipatia vikundi vingine ili kufikia asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotakiwa kisheria.

2.10.2 Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF) awamu III.

Utekelezaji wa mpango wa TASAF III katika Wilaya ya Simanjiro ulianza Julai **2015**. Hadi kufikia Desemba **2016** wilaya ilikuwa na jumla ya Walengwa **4,025**. Jumla ya kaya **39** zilitolewa kwenye Mpango kwa sababu mbalimbali zikiwemo kuhama, vifo kwa walengwa wasio na wategemezi, na walioingia kwenye Mpango kimakosa.

Katika utekelezaji wa agizo la serikali la uhakiki upya wa kaya zinazonufaika na Mpango wa TASAF III nyumba kwa nyumba, jumla ya mitaa kumi na moja **(11)** imehakikiwa katika kata ya Mirerani, Endiamtu na Orkesumet. Jumla ya wanufaika **116** wamebainika kuwa hawakustahili kuingizwa kwenye mpango na hivyo wameshaondolewa kwenye malipo ya mwezi Januari na Februari **2017** na kuandikiwa barua za kurejesha fedha. Zoezi la uhakiki linaendelea katika maeneo mengine yaliyobaki ili kufikia mwezi Machi 2017 taarifa kamili iweze kupatikana. Inatarajiwa kiasi cha shilingi **40,252,000** zilizotolewa kwa wanufaika waliokosa sifa na kuondolewa kwenye malipo zitarejeshwa. Wahusika wameshaandikiwa barua na ufuatiliaji unafanyika kupitia maafisa watendaji wa ijiji na kata.

2.11 SEKTA YA ARDHI NA MALIASILI.

2.11.1 Usimamizi na matumizi bora ya ardhi

Lengo kubwa la sekta ya ardhi na maliasili ni kusimamia mgawanyo ulio sawa na wa haki wa rasilimali za ardhi, misitu na wanyamapori pamoja na matumizi endelevu baina ya watumiaji mbalimbali. Wilaya imefanya jitihada za kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kupitia mikutano ya vijiji kuhusu sheria za ardhi na matumizi bora ya rasilimali za misitu na wanyamapori, pamoja na kuhamasisha wadau kuchangia jitihada za upimaji wa ardhi na utatuzi wa migogoro pale inapojitokeza.

Kati ya vijiji **57** vya wilaya, vijiji **41** vimebainishwa mipaka yake na kati yake vijiji **11** vina vyeti vya ardhi ya kijiji. Hata hivyo, licha ya vijiji kubainishwa mipaka yake na kuwa na vyeti bado kumekuwa na migogoro ya mwingiliano wa mipaka. Vijiji vingi havijaunda mabaraza ya ardhi ya vijiji na yale yaliyopo hayafanyi kazi ipasavyo. Kwa upande wa mabaraza ya kata, **15** kati ya **18** yanafanya kazi na hivyo kupunguza migogoro na msongamano wa mashauri katika baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ambalo linafanya kazi nzuri.

Kwa upande wa matumizi bora ya ardhi, vijiji **19** kati ya **57** vimefanikiwa kuandaa na kutekeleza mpango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji kulingana na sheria ya matumizi ya ardhi namba **8** ya mwaka **2007**. Mipango hiyo imepunguza kwa kiasi kikubwa migogoro iliyokuwepo hasa ya mwingiliano wa matumizi kati ya wakulima na wafugaji kwenye kijiji cha Kitwai A na B, Londrekes, Lerumo na Ruvu Remit.

2.11.2 Migogoro kati ya vijiji na vijiji

Kwa kipindi cha mwaka 2012 hadi 2016 kumekuwa na migogoro ya ardhi baina ya vijiji ikihusisha vijiji vya Emboreet na Lobosireet, Emboreet na Lobosoit A, Emboreet na

Sukuro pamoja na Kityangare na Sukuro. Migogoro mingine imehusisha vijiji vya Orkesumet na Endonyongijiape, Namalulu na Narakauo, Kityangare, Narakauo na Lobosiret. Katika kukabiliana na migogoro hii, Wilaya iliamua kutoa mafunzo kwa wenyeviti na watendaji wote wa vijiji pamoja na watendaji wa kata tarehe **29-30 Septemba 2016**, ili wazingatie sheria, kanuni na taratibu katika maamuzi yanayohusu ardhi. Aidha, uongozi wa wilaya umefika katika vijiji vyenye migogoro na kuzungumza na serikali za vijiji ambazo zimetumia elimu hiyo kukabiliana na migogoro kati ngazi ya kijiji kabla haijafika wilayani. Elimu hii pamoja na jitihada za uongozi wa wilaya vimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro kuanzia mwezi Oktoba 2016.

2.11.3 Migogoro kati ya wilaya na wilaya nyingine

(i) Lobosoit A vs Loksale

Mgogoro wa mipaka kati ya kijiji cha Lobosoit A cha Simanjiro na kijiji cha Loksale kilichoko wilaya ya Monduli umedumu tangu 2015 licha ya jitihada za wilaya zote mbili kutafuta suluhu ya kudumu. Ili kupata suluhu ya kudumu, yamefikiwa makubaliano ya pande zote mbili na kuunda timu za wilaya na mkoa kufanya majadiliano ya pamoja kufikia mwisho wa mwezi Februari 2017. Timu za wilaya na Mkoa zitahusisha kamati za ulinzi na usalama na wataalamu wa idara za ardhi na maliasili.

(i) Kitwai B vs Gitu

Mgogoro huu umedumu kuanzia mwaka 2015 ukihusisha ugomvi wa mipaka kati ya vijiji vilivyo kwenye mpaka wa wilaya za Simanjiro na Kilindi mkoani Tanga. Watendaji wa halmashauri zote mbili wamejaribu kusuluhisha bila kufikia muafaka. Kwa sehemu kubwa mgogoro umechochewa na wakulima walioondolewa kutoka hifadhi ya jamii ya Emborey Murtangos iliyoko Kiteto. Ili kupata suluhu ya kudumu, yamefikiwa makubaliano ya pande zote mbili ya kuunda timu za wilaya na mkoa kufanya majadiliano ya pamoja kufikia mwisho wa mwezi Februari 2017. Timu za wilaya na Mkoa zitahusisha kamati za ulinzi na usalama na wataalamu wa idara za ardhi na maliasili.

2.11.4 Migogoro kati ya Wilaya na hifadhi ya Taifa

Katika Wilaya ya Simanjiro kuna baadhi ya vijiji vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Pori la Akiba la Mkungunero na Vijiji hivyo vilipimwa na kupatiwa hati mnamo mwaka 1991 na vingine Mwaka 2000. Kijiji cha Kimotorok kinapakana na Pori la Akiba la Mkungunero na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Hifadhi ya Taifa Tarangire ilitafsiri ardhini Tangazo la Serikali namba 160 la mwaka 1970 mnamo mwaka 2004 kwa kuwatumia wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi na Mandeleo ya Makazi, Idara ya upimaji na Ramani (SMD). Tafsiri hiyo ilibaini muingiliano wa kiutawala na kiutendaji baina ya Wilaya za Kondoa, Kiteto na Simanjiro.

Katika kutatua matatizo ya muingiliano huo, vikao mbalimbali vya kutatua matatizo/migogoro vimefanyika kwa ngazi ya Mkoa wa Manyara na Dodoma pia kuwahusisha Wakuu wa Wilaya za Kondoa, Kiteto na Simanjiro na kuandaliwa taarifa ya mapendekezo pamoja kuhusu matatizo ya mipaka hiyo. Taarifa hiyo iliwasilishwa

kwa Wakuu wa Mikoa ya Dodoma na Manyara kwa hatua zaidi za ufumbuzi. Baada ya taarifa ya mapendekezo kuwasilishwa kwa Wakuu wa Mikoa ya Dodoma na Manyara, iliagizwa iundwe timu ya wataalam itakayofanya kazi ya kutathimini na kubainisha hali ya mgogoro na kutoa mapendekezo ya kitaalamu yatakayotoa suluhisho la migogoro ya maeneo ya hifadhi ya Taifa Tarangire na wilaya za Kondoa, Kiteto na Simanjiro.

Mwaka 2014 ofisi ya Waziri Mkuu iliunda timu ya utatuzi wa mgogoro baina ya wananchi wa maeneo ya Hifadhi Tanzania. Kazi iliyofanyika ni kupitia matangazo yote ya serikali ya mipaka na ramani zote za upimaji na kuzitafsiri ardhini. Timu hiyo ya wapima ardhi ilifanya kazi ya kutengeneza mpaka mpya kulingana na matangazo yote ya serikali na ramani zote za upimaji na kukubaliana na uongozi wa serikali za vijiji husika na baada ya hapo mapendekezo yalipelekwa kwa Waziri Mkuu kwa ajili ya maamuzi, hivyo wilaya inaendelea kusubiri maamuzi ya ripoti ya timu ya wataalam.

Wilaya imeweka mikakati ya kukabiliana na tatizo la ukuaji na ujenzi holela wa miji ya Orkesumet na Mirerani pamoja na vijiji-miji vinavyokua kwa kasi kwa kupima na kumilikisha viwanja. Wilaya imebainisha eneo na kuandaa michoro na ramani katika mji mdogo wa Mirerani ambako viwanja **421** vinapimwa hadi kufikia mwisho wa mwezi Februari 2017. Viwanja hivi vitauzwa kwa bei ya kawaida kwa wananchi na vinatarajiwa kuiingizia halmashauri ya wilaya takribani shilingi **bilioni 1.** Jumla ya vijiji-miji sita vinavyokua kwa kasi vimebainishwa tayari kwa upimaji kuanzia mwaka wa fedha 2017/18. Vijiji hivyo ni Naisinyai, Losinyai, Terrat, Komolo, Naberera na Nyumba ya Mungu. Upimaji huu utapunguza migogoro kati ya wamiliki wa ardhi mijini na kuwapa uhakika wamiliki wa ardhi husika.

2.11.6 Wanyamapori na misitu

Sekta ya wanyama pori na misitu ina lengo la kukuza uhifadhi wa maliasili na kukabiliana na uharibifu wa mazingira na uwindaji haramu. Hatua zinazochukuliwa na wilaya katika kukabiliana na ujangili na uharibifu wa mazingira ni pamoja na kuendesha doria za mara kwa mara kwenye maeneo ya hifadhi za wanyamapori na misitu, kushirikiana na wadau wa uhifadhi na uwindaji endelevu kukabiliana na wawindaji haramu. Baadhi ya wadau ni pamoja na:- Kikosi dhidi ya Ujangili kanda ya Kaskazini (KDU), TANAPA na Kampuni za Uwindaji zilizopo ambazo ni TAWISA, ESHKESH SAFARIS, AFRICAN TRADITION SAFARIS, MELAMI HUNTING SAFARIS, MWATSI SAFARIS, TANZANIA BUNDU SAFARIS, BUNDA SAFARIS, WEMBERE SAFARIS, HSK SAFARIS. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2016, majangili 10 walikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali mahakamani.

Aidha, jumla ya kambi **58** ndogo ndogo za wachoma mkaa ziliteketezwa na zaidi ya magunia **2,400** ya mkaa yalikamatwa na kuuzwa katika vijiji vya Namalulu, Lorbene, Losokonoi, Orchoronyori na Okutu.

2.11.7 Ufugaji wa nyuki

Wilaya imeendelea na zoezi la uhamasishaji wa jamii katika ufugaji wa kisasa wa nyuki. Uhamasishaji huo unaendelea katika maeneo mbalimbali wilayani ikiwa ni pamoja na usambazaji wa mizinga ya nyuki na vifaa vya kurinia asali pamoja na utengaji wa maeneo ya vijiji ya ufugaji wa nyuki. Kwa sasa, wilaya ina jumla ya vikundi **96** vya ufugaji nyuki na jumla ya mizinga **4,283** kati yake mizinga **1,274** ni ya kisasa na mizinga **3,009** ni ya asili.

2.11.0 CHANGAMOTO

Wilaya inakabiliwa na changamoto mbali mbali katika kuhakikisha inawaletea Maendeleo wananchi kwa wakati, baadhi ya changamoto hizi ni hizi zifuatazo:-

- Upungufu wa rasilimali watu, fedha pamoja na vitendea kazi ukilinganisha na ukubwa wa eneo la wilaya.
- Upungufu wa maji kwa ajili ya matumzi ya binadamu, mifugo na ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama vile barabara na majengo
- Upungufu wa Walimu kwa shule za msingi na sekondari ambao unatokana na mgao wa Walimu kwa kutumia hesabu za uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi badala ya mikondo. Shule nyingi zina wanafunzi pungufu ya 280 hivyo kiuwiano, Wilaya inaonekana kuwa na walimu wa kutosha lakini kimkondo ina upungufu mkubwa. Mahitaji ya walimu kwa shule za msingi ni **321** na kwa sekondari ni walimu **83** wa sayansi tu.
- Kukosekana kwa gereza la wilaya kumepelekea kuwepo kwa gharama kubwa za kusafirisha mahabusu na wafungwa kupelekwa Kiteto.
- Upungufu wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari hasa mahitaji ya madarasa, hosteli na mabwalo kwa shule za sekondari kwasababu shule zote huendeshwa kwa mtindo wa shule za bweni badala ya kutwa kutokana na umbali wa makazi ya wananchi na ziliko shule.
- Ukosefu wa hospitali ya wilaya, hivyo kutegemea Hospital binafsi na Vituo vya afya na Zahanati. Panapotokea *kesi* kubwa mgonjwa hulazimika kupelekwa Hospital ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha.
- Utoroshaji wa madini ya Tanzanite na uuzwaji nje ya wilaya unaoikosesha halmashauri mapato yatokanayo na biashara hiyo.
- Wachimbaji wengi wa madini kutokutoa takwimu sahihi za uzalishaji zinazoiwezesha halmashauri kukusanya kodi ya huduma.
- Hati asilia ya madini ya Tanzanite kuendelea kuwa na jina la Arusha badala ya Simanjiro-Manyara na hivyo kuikosesha Halmashauri mapato ya biashara yatokanayo na hati hiyo

2.11.1 MIKAKATI

Hata hivyo Wilaya inaendelea kuhakikisha inasimamia upatikanaji wa maendeleo ya wananchi kwa kukabiliana na Chngamoto hizo kupitia mikakati ifuatayo:-

- Wilaya imetoa taarifa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti Utumishi wa Umma juu ya upungufu wa watumishi kwa ajili ya kupewa kibali cha ajira., Halmashauri inaendelea kufuatilia kibali hicho sawa na ilivyoainishwa katika bajeti ya **2016/2017**
- Kupanga na kufanya matengenezo ya barabara kipindi mvua zinapoelekea kwisha.
- Kuanzisha jukwaa la wadau wa maendeleo na mfuko wa maendeleo ya wilaya ili wadau mbalimbali waweze kuchangia shughuli za maendeleo.
- Kuendelea kushirikisha wadau na kutafuta wahisani mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa mioundombinu kama vile mabwalo, nyumba za walimu na vyoo
- Wilaya inaendelea na upanuzi wa kituo cha afya cha Urban Orkesumet kwa lengo la kuipandisha kuwa hospitali ya Wilaya. Kwa mwaka 2016/17 wilaya imetenga jumla ya shilingi **milioni 80** kutokana na fedha za ruzuku ya maendeleo (CDG) kwa ajili ya hospitali hii, na katika bajeti ya mwaka 2017/18, wilaya imependekeza kutenga shilingi **milioni 620** kukidhi lengo hilo.
- Halmashauri imeandika barua kwa Waziri wa Nishati na Madini ili kupata "HATI ASILIA" (Certificate of Origin) ya Tanzanite ambayo kwa sasa inasomeka kuwa Tanzanite inapatikana Mirerani Arusha Tanzania badala ya Mirerani Manyara Tanzania. Hivyo itasaidia kuongezwa kiwango cha malipo ya kodi ya Huduma.
- Kukusanya kodi ya majengo katika Mji Mdogo wa Orkesumet na Mirerani baada ya kukamilika kwa sheria ndogo ya kodi ya majengo 'Property Tax'.
- Kuendelea kushirikiana kwa karibu na wakala wa ukaguzi wa madini (TMAA) ili kuipatia halmashauri takwimu za mauzo ya madini kutoka kwenye makampuni mbalimbali kwa wakati.

2.12. HITIMISHO

Kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha taarifa hii ya maendeleo ya wilaya ikibainisha mafanikio kadhaa katika utekelezaji wa maendeleo, iliyozingatia dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Malengo ya maendeleo endelevu, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016-2020, maelekezo ya mheshimiwa Rais waJamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika hotuba yake wakati wa ufunguzi wa Bunge la kumi na moja na sera mbalimbali za uchumi na huduma za jamii. Pamoja na kukabiliwa na changamoto mbalimbali, uongozi wa wilaya umeweka jitihada za kutosha kuhakikisha maendeleo yenye mguso kwa maisha ya wananchi yanapatikana. Ni matumaini yangu kuwa uongozi wa kitaifa wa awamu ya tano ambao umejipambanua kwa kauli mbiu ya **HAPA KAZI TU** utaendelea kuunga mkono jitihada hizi za uongozi wa wilaya ya Simanjiro.

Naomba kuwasilisha

Mhandisi Zephania A.D Chaula
Mkuu wa Wilaya
Simanjiro